

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 6: “Dead End”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: DAY AT ASKALE’S HOME

- **Askale (f,21)**
- **Samy (m, 6)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: DAY AT PAPA TILAHUN'S COMPOUND

- **Aster: (f, 15)**
- **Papa Tilahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE THREE: DAY IN THE LOCAL MARKET

- **Askale (f,21)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR:NIGHT IN THE VILLAGE

- **Jonas (m, 15)**
- **Mekete (m, 16)**
- **Challa (m, 17)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa watazamaji! Huu ni mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako unaoitwa “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Sasa hivi, tunaisikiliza sehemu ya sita inayoitwa “KUGINGA MWAMBA”. Katika sehemu iliyopita, mvulana mdogo Begidu alikuwa ametoweka kwa muda wa kiasi wiki moja hivi. Aster, mjukuu wake Papa Tilahun, aliingiwa na wasiwasi alipopokea habari kuhusu Begidu kwa njia ya simu. Je ilikuwa habari gani? Tutajua hayo hivi karibuni. Lakini kwanza hebu tuungane na Askale nyumbani kwake akimbembeleza mwanawe Samy ambaye amehuzunika kwa rafiki yake kutoweka.

SCENE ONE: DAY AT ASKALE’S HOME

1. SFX: TEA BOILING

2. **Samy:** Mama, Lini watampata Begidu?
3. **Askale:** Sina hakika, Samy, lakini watampata.
4. **Samy:** Kwani mimi ndiye niliyemsababisha Begidu kutoweka?

KW Beginn

5. **Askale:** Hapana, Samy, nani kasema hivyo?
6. **Samy:** Hakuna! Lakini ametoweka punde baada ya mimi kupigana naye. Lau sikumpiga, pengine

asingetoweka.

KW Ende

7. **Askale:** Samy, mwanangu, hakutoweka kwa sababu yako wewe. Usijilaumu kwa hilo. Lakini usirudie tena kupigana naye.

8. **Samy:** Sawa ma! Sitapigana tena.

9. **Askale:** Mtoto mzuri. Nina hakika polisi watampata Begidu hivi karibuni, kwa hivyo usiwe na wasiwasi. Sasa kula kiamshakinywa.

10. **Samy:** Lakini mama, wakati Begidu atakaporudi, ni sawa nikienda kwake kumuomba msamaha?

11. **Askale:** Naam! Jambo zuri hilo! Tutakwenda pamoja.

12. SFX: TEA POURING IN A CUP

13. **Askale:** Chai yako hii hapa.

14. SFX: CUP BEING PUT ON THE TABLE

15. **Askale:** Na huu mkate niliuoka leo asubuhi. Na matunda ya kukupa vitamini.

16. SFX: PLATE BEING PUT ON THE TABLE

17. **Samy:** Asante mama, mama!

18. **Askale:** Si neno, mwanangu!

19. **Samy:** Kwani wewe huli, ma?
20. **Askale:** Naam, nitakula. Lakini mimi nitakusimulia hadithi wakati unapokula kiamshakinywa.
21. **Samy:** **(Curiosity)** Ma, utanisumulia hadithi kuhusu “fisi mpumbavu mlafi na nyani mwerevu”?
- KW Beginn**
22. **Askale:** **(Happy)** Mara nyingine unanistaajabisha na huo werevu wako. Unaweza kusimulia hiyo hadithi?
23. **Samy:** **(He recites the fable)** Jua liliendelea kutoka taratibu huku likitoa miale miekundu...
24. **Askale:** Mashallah! Hujasahau hata kidogo mwanzo wa hadithi ingawa nilikusimulia juma lililopita.
25. **Samy:** Ghafla, nyani alitazama chini akaona fisi mpumbavu na mlafi akikimbia kupitia shambani akielekea pangoni mwake. Alitaka kufika kwenye pango lake, lenye kiza kabla ya jua kutoka kabisa. Nyani alicheka kwa sauti kubwa alipomwona fisi jinsi alivyokuwa akikimbia.
26. **Askale:** Hongera sana mwanangu; wewe ni mwerevu kweli!

27. **Samy:** Naam, ma. Lakini mama, mbona huyo fisi alikuwa na mwendo wa ajabu?
28. **Askale:** Sawa! Mtazame, fisi ana miguu minne, ya nyuma ni mifupi kuliko ya mbele; ndiyo sababu fisi ana mwendo usiolekea.
29. **Samy:** Nimefahamu, ma!
30. **Askale:** Haya, sasa, acha nikumalizie hadithi.
31. **Samy:** Sawa, ma!
32. **Askale:** Fisi hakushughulika bali alimtazama nyani kwa hasira kisha akaendelea na mbio zake. Nyani akacheka tena.

KW End

Fisi aliapa moyoni mwake: “Nitamkamata huyo nyani hivi karibuni na nitamla!” Siku chache baadaye, fisi akamuona nyani akicheza ardhini; wala nyani hakumuona. Fisi alikimbia kisirisiri akamvamia nyani kutokea nyuma! Nyani alianza kutetemeka kwa hofu, na akamwambia fisi: “Mwenzangu unanifanya mwili wangu wote uzizime.” Fisi alicheka na kumwambia nyani kwa kejeli, “ Nakuona jinsi unavyotetemeka kwa hofu!”

33. **Samy:** Maskini, nyani!
34. **Askale:** Kuwa na subira. Samy, unaweza kukisia kile

ambacho nyani anamwambia fisi?

35. **Samy:** Pengine, anamwambi, "usinile, Bi mkubwa"?

36. **Askale:** Angesema hivyo lakini nyani ni mwerevu sana. Alisema: "Aaa nawe bi mkubwa, tazama kule, kuuvuka ule mlima. Chakula cha huko ni bora zaidi. Wajua ua wa kule si wa mawe na mbao; ua wenyewe umejengwa kwa matumbo na chango!" Fisi alishawishika kwa maneno na akakimbia kadiri ya uwezo wake ili apate chakula kizuri zaidi. Lakini alirudi mkono mtupu.

37. **Samy:** **(Laughs).**

KW begin

38. Askale: **(Laughs)** Fisi akazidisha hasira. Siku chache baadaye akamkamata nyani kwa mara ya pili: “Sasa nitakutafuna mara moja! Nimetafuta chakula usiku na mchana na hapa nilipo nina njaa ajabu,” fisi alisema kwa hasira. Nyani hakuonyesha kushtuka “Bibiye pole sana kwa kukosa kitu cha kula. Kama unataka kunila, ninakushauri unirushe juu kisha ufungue kinywa chako kadiri ya uwezo wako! Hapo nitatumbukia moja kwa moja tumboni mwako wala sitakwama kwenye koo yako!” Fisi mpumbavu na mlafi akakubali akamrusha nyani hewani. Nyani alidaka tawi la mti lililokua karibu, akaruka kuondoka na hatari huku alimcheka fisi mpumbavu. Alikuwa amemcheza shere fisi mara mbili. Kutoka wakati huo, nyani akawa anaishi kwa tahadhari. Je Samy mwanangu umeielewa hadithi hii?

KW end

39. Samy: Nyani alikuwa mpumbavu sana naye nyani alikuwa mwerevu sana.

40. Askale: Asante! Maanake nini?

41. Samy: Maanake, tusiwe wapumbavu kama fisi.

42. Askale: Naam. Usiwe mpumbavu na mlafi kama fisi. Ni lazima pia uwaheshimu wenzako.

43. **Samy:** Sawa, ma.
44. **Askale:** Nitakusimulia hadithi nyingine kesho. Unataka nikuongezee chai?
45. **Samy:** Hapana, asante ma.
46. **Askale:** Sawa! Ebu nisaidie kuzipeleka hizo jikoni.

47. **SFX: PICKING PLATE AND GLASSES**

48. **NARRATION:** Samy anasikika mwenye furaha baada ya kusimuliwa hadithi. Kwa kweli, wataalamu wengi wanaamini kwamba watoto wanapozisikiliza hadithi hupata maarifa ya kujieleza kwa ufasaha. Muundo mwepesi wa hadithi unawafanya watoto kufahamu maelezo muhimu. Kutamba hadithi za kienyeji husaidia kutoa habari na pia husababisha mijadala jinsi tulivyoona leo kati ya Askale na mwanwe, Samy. Bara la Afrika lina utajiri mkubwa wa hadithi za kienyeji, kwa hivyo ni muhimu kuuhifadhi utamaduni huo adhimu.

SCENE TWO: DAY AT PAPA TILAHUN'S COMPOUND

49. **SFX: PLOUGHING THE GARDEN BY HAND**

50. **Mama Beletu:** **(Ploughing the garden by hand)** Balaa hii!
Shamba lote limejaa kwekwe!
51. **Aster:** **(Arrives, delighted)** Bibi! Ninajua tunakoweza
kumpata Begidu.
52. **SFX: STOP PLOUGHING**
53. **Mama Beletu:** Ati wasema nini? Umempata Begidu?
54. **Papa Tilahun:** **(From inside the room)** Kuna nini?
55. **Mama Beletu.** **(Replies him loudly)** Anasema ati amempata
mtoto aliyetoweka.
56. **Aster:** Bibi!
57. **Papa Tilahun:** **(Approaching)** Amempata nani?
58. **Mama Beletu:** Amempata Begidu.
59. **Aster:** Bibi, nimesema, Najua tunakoweza kumpata
Begidu. Sijasema nimempata.
60. **Papa Tilahun:** **(Laughs sarcastically)** Alaa! Beletu, unazidi
kukomaa kila kukicha.
61. **Mama Beletu:** Na wewe unazidi kuwa mchanga kila kukicha **(all
laugh)**.
62. **Aster:** Babu, ninakuahidi, hivi karibuni tutampata Begidu.
63. **Papa Tilahun:** Basi, tuambie tutampata wapi?

64. SFX: ASTERS CELLPHONE RINGING

65. Aster: (In a hurry) Nitawaeleza kwa kina baadaye; naomba nijibu simu hii. Ni rafiki yangu wa dhati, Semira (**walks away**).

66. SFX: FOOTSTEPS LEAVE

67. Aster: (**Picks up call from a distance**) Hallo! Semira...

68. NARRATION: Aster anaelekea kuwa na wasiwasi sana kumhusu Begidu. Je huenda sababu yake ni kwamba anampenda Jonas, mjombake Begidu? Naam, kwa namna fulani, hayo ni kweli, lakini kuna sababu nyingine. Katika mataifa mengi barani Afrika, watoto wengi huishi na babu na bibi zao. Kuna sababu kadha wa kadha. Pengine wazazi walifariki duniani, pengine mama yao asiye na mume hawezi kuwatunza vyema au pengine ndoa ya wazazi wao imevunjika. Aster anatunzwa na babu na bibi yake na yeye anataka kuwasaidia pia. Twendeni sasa sokoni ambapo marafiki wawili Kassech na Askale wanafanya kazi.

SCENE THREE: DAY IN THE LOCAL MARKET

69. SFX: MARKET AMBIENCE

70. ATMO: MANY PEOPLE IN THE MARKET

71. **Kassech:** Hapana, wazazi wa wazazi wangu walifariki dunia kitambo sana.
72. **Askale:** Na babako je? Tayari umeshaniambia habari za mamako.
73. **Kassech:** Simjui babangu lakini najua yu hai. Punde baada ya kifo cha mamangu nilipata ujauzito nikamzaa mtoto asiye kuwa na baba kama mimi (**she laughs sarcastically**). Maisha yangu yana vituko, rafiki yangu.
74. **Askale:** Yangu pia, mwenzangu.
75. **Kassech:** Wajua kosa nililolitenda? Nilimwamini mpenzi wangu sana.
76. **Askale:** Kwa nini akakusaliti?
77. **Kassech:** Anatoka kwenye familia ya kihafidhina, na aliniambia familia yake haikukubali ujauzito wangu na uhusiano wetu. Tena nilikuwa mtoto sana wala sikuwa na tajiriba yoyote ya maisha. (**she inhales deeply and exhales**).
78. **Askale:** Huo umri ulikuwa hatari sana kwetu sisi wawili; wala hatuwezi kubadilisha hali ya mambo sasa.
79. **Kassech:** Kweli! Hatuwezi kubadilisha hali ya mambo, lakini

kuna jambo moja ambalo bado twaweza
kulifanya. Hatutakuwa wategemezi wa wanaume
tena!

80. **Askale:** Naam! Kwa sababu sisi ni wanawake wenye
nguvu.

81. **NARRATION:** Naam, wanapaswa kuwa kina mama wenye uwezo.
Askale amemwambia Kassech kuhusu maisha yake ya hapo
awali na visa vyao vinafanana sana – na pia vinafanana sana na
vya vijana wengine wa Kiafrika. Askale alipotambua kuwa
alikuwa mjamzito, alitoroka nyumbani kuepukana na dhiki za
wazazi wake; na wakati huo huo, mpenzi wake akamtelekeza.

SCENE FOUR: NIGHT IN TOWN

82. **SFX: NIGHT AMBIENCE**

83. **Jonas:** Nadhani tumekumbuka kila kitu.

84. **Challa:** Kila kitu!

85. **Mekete:** Visu?

86. **Challa:** Ninavyo!

87. **Mekete:** Jonas, una kamba?

88. **Jonas:** Naam!

89. **Mekete:** Na bastola bandia?
90. **Challa:** Tuna kila kitu!
91. **Mekete:** Naam, nadhani tumejiandaa vya kutosha.
92. **Jonas:** Ndiyo!
93. **Mekete:** Na kipande cha nyama yenye sumu?
94. **Jonas:** Cha nini kipande cha nyama yenye sumu?
95. **Mekete:** Cha nini...!? Si wewe uliyetuambia mara iliyopita kwamba huyo jamaa ana mbwa mkali sana nyumbani kwake!
96. **Jonas:** Loo!, naam, naam! Samahani, nimesahau kabisa.
97. **Challa:** Maanake leo wizi hakuna.
98. **Mekete:** Balaa! Tukutane kesho alasiri kwenye baa yetu ya kila mara; na tuisahau kuleta kila kitu.

KW Beginn

99. **Mekete:** Kila kitu kwa maana ya kila kitu, isipokuwa mbwa huyo wako mpumbavu!

100.SFX: DOG APPROACHES, BARKING

101.Challa. (Throws a stone and hit the dog).

102.SFX: DOG WHINES AND RUNS AWAY

KW Ende

OUTRO:

Je! hao vijana watatu watajitosa kwenye uhalifu? Kwa haya na mengine, tegea sikio sehemu ijayo ya mchezo wetu, **“Mwana Mpotevu- Kisa cha kina mama wawaleao watoto wao bila baba zao barani Afrika”**. Kumbuka, ukitaka kuisikiliza sehemu tena au kuwasilisha maoni na mapendekezo nenda kwenye ukurasa wetu wa tovuti dw.de/lbe. Kwaheri!